



*Habari kwa Jamii za Tamaduni Mbalimbali*

## **KITUO CHA AFYA CHA MATIBABU YA TAMADUNI MBALIMBALI CHA QUEENSLAND (QTMHC)**

Huduma ya Madawa ya kulevya ya Metro Kusini na Afya ya Akili (MSAMHS)

### **Sisi ni nani:**

Sisi ni huduma ya kitaaluma ya mkoani kote ambayo inafanya kazi ili kuhakikisha watu kutoka kwa asili tofauti za kitamaduni wanapata huduma na msaada wa afya ya akili na kwamba huduma wanazozipata zinaitikia mahitaji yao binafsi.

### **Gharama:**

Hakuna gharama yoyote

### **Maeneo tunayoyahudumia:**

Maeneo yote katika Queensland

### **Watu tunaofanya kazi nao:**


- watu kutoka asili mbalimbali za kitamaduni na lugha
- watu wa umri wote
- watu ambao wana matatizo ya kihisia, kijamii, au kisaikolojia
- wanafamilia wa watu ambao wana matatizo ya afya ya akili na wanapokea huduma ya afya ya akili na msaada
- watoa huduma ambao wanahusika katika huduma na matibabu ya watu walio na matatizo ya afya ya akili
- makundi ya jamii ya kitamaduni kusaidia kuboresha uelewa kuhusu afya ya akili na ustawi na huduma zinazopatikana

### **Ruhusa:**

Ruhusa kutoka kwa mtu mwenye shida ya afya ya akili inapaswa kupatikana ili sisi tuweze kufanya kazi moja kwa moja na mtu huyo. Ruhusa kutoka kwa mtu pia ni muhimu ikiwa tunatakiwa kufanya kazi na wanafamilia. Ikiwa mtu huyo ni hatari kwa mwenyewe au kwa wengine, tathmini inaweza kutolewa bila ridhaa kupitia Sheria ya Afya ya Akili 2016.

### **Tunachokifanya:**

- Tunatafuta kuelewa ufafanuzi wa kitamaduni (ikiwa ni pamoja na dini) na athari za utamaduni juu ya matatizo ya afya ya akili. Hii husaidia wauguzi wa afya ya akili wakati wa kufanya maamuzi kuhusu matibabu na huduma.
- Tunatoa taarifa kuhusu afya ya akili kwa watu binafsi na familia ili kuwasaidia kuelewa vizuri ugonjwa wao na jinsi ya kukabiliana nayo.

- 
- Tunatoa mafunzo na kutafuta watu wa kujitolea katika makundi ya jamii ya kitamaduni ili kusaidia kushughulikia unyanyapaa juu ya ugonjwa wa akili na kujiua, kuongeza ujuzi wa kukabiliana na wasiwasi wa kurekebisha utamaduni mpya, na kuboresha ujuzi kuhusu huduma za afya ya akili.
  - Tunaendesha vikao vya elimu ya jamii juu ya magonjwa ya akili na mada ya afya, yaani jinsi viongozi wa jumuiya wanaweza kusaidia usaidizi wa watu kwa huduma.
  - Tunaendeleza na kushirikiana habari kuhusu afya ya akili na ustawi katika lugha nyingi.

#### **Nini kinatufanya sisi kuitikia kiutamaduni?**

Tuna wafanyakazi wa kitamaduni kutoka kwa makundi zaidi ya 160 ya kitamaduni na lugha. Tunawaunganisha wafanyakazi hawa kwa watoa huduma za afya ya akili ili waweze kusaidia kuwajulisha huduma za afya ya akili.

#### **Wasiliana nasi:**

***Mtu yeyote anaweza kutaja QTMHC (ikiwa ni pamoja na watu binafsi, wana familia, au watoa huduma)***

Simu: (07) 3317 1234 OR 1800 188 189 (Nje ya maeneo ya mji wa Brisbane)

Masaa ya kazi: Jumatatu hadi Ijumaa 8:30 am mpaka 4:30 pm

Anwani: Level 2, 228 Logan Road Woolloongabba QLD 4102

Barua pepe: [QTMHC@health.qld.gov.au](mailto:QTMHC@health.qld.gov.au)

Tovuti: <https://metrosouth.health.qld.gov.au/qtmhc>